Ninaweza kufanya nini kingine?

Hata kama unazo mamogramu za mara kwa mara, BreastScreen SA inawahimiza wanawake wote “kuwa na ufahamu wa matiti”. Kama utagundua mabadiliko yoyote yasiyo ya kawaida katika matiti yako, weka miadi ili kuweza kumuona daktari wako wa kila siku bila kuchelewa. Kumbuka ugunduzi wa mapema ni muhimu sana!

Ninaweza kufanyiwa uchunguzi wa mamogramu wa bure wapi?

Kliniki za BreastScreen SA zinapatikana katika:

- **Arndale**
  Centro Arndale, Shop 29 C facing Hanson Road, Kilkenny
- **David Jones Rose Clinic**
  Lower Ground Floor, Adelaide Central Plaza, 100 Rundle Mall, Adelaide
- **Adelaide (Frome Road)**
  Gate 4 or 5, University of SA Campus, opposite the Dental School
- **Christies Beach**
  107-109 Dyson Road, Christies Beach
- **Elizabeth**
  GP Plus Health Care Centre, 16 Playford Boulevard, Elizabeth
- **Hyde Park**
  292-294 Unley Road, Hyde Park
- **Marion**
  Suite 6 Marion Medical Centre, 199 Sturt Road, Seacombe Gardens

BreastScreen SA pia ina Vitengo Sogevu vya Uchunguzi ambavyo vinatembelea maeneo ya nchi kila baada ya miaka miwili.

Ili kuweka miadi, piga nambari 13 20 50.

Barua ya pendekezo kutoka kwa daktari haihitajiki, na huduma za bila malipo za ukalimani zinapatikana. Kuhifadhi nafasi ya kundi pia kunapatikana kwa wanawake ambao wangependa kuhudhuria kwa kundi.

For more information

BreastScreen SA
SA Health
Telephone: 13 20 50
www.sahealth.sa.gov.au/breastscreen
bssaenquiries@health.sa.gov.au

If you do not speak English, request an interpreter from SA Health and the Department will make every effort to provide you with an interpreter in your language.

BY NC ND
www.ausgoal.gov.au/creative-commons

© Department of Health and Ageing, Government of South Australia. All rights reserved. Printed March 2014. 13037

Government of South Australia
SA Health

Taarifa ya uchunguzi wa matiti kwa wanawake

Government of South Australia
SA Health

Saratani ya matiti ndiyo saratani maarufu zaidi inayogunduliwa miongoni mwa wanawake, huku mwanamke mmoja kati ya kumi katika eneo la Australia Kusini akigunduliwa kabla ya umri wa miaka 75.

Saratani ya matiti haiwezi kuzuiliwa lakini kinga bora zaidi kwa mwanamke ni ugunduzi wa mapema.

Saratani ya matiti – hoja

Saratani ya matiti ni kundi la seli zisizo za kawaida ambazo zinaendelea kukua na kuongezeka. Hatimaye seli hizi huenda zikaunda dude katika titi. Kama saratani hiyo haitaondolewa au kudhibitiwa basi seli hizo za saratani zinaweza kuenea katika viungo vingine vya mwili na hata kusababisha kifo. Kugundua saratani ya matiti katika awamu ya mapema kunaboresha uwezekano wa matibabu yenye ufanisi.

Hali za hatari kubwa zaidi za kuanza kuwa na saratani ya matiti ni kuwa mwanamke na kuanza kuzeeka. Zaidi ya 75% ya saratani za matiti zinagunduliwa miongoni mwa wanawake walio na umri wa miaka 50 na zaidi.

BreastScreen SA inatoa uchunguzi wa bila malipo wa mamogramu (Eksirei ya matiti) kwa wanawake walio na umri wa miaka 40 au zaidi wasiona dalili zozote kwenye matiti. Wanawake wote, haswa walio na umri wa kati ya miaka 50 na 69 wanahimizwa kuweza kufanyiwa uchunguzi wa bila malipo wa mamogramu kila baada ya miaka miwili.

Uchunguzi wa mamogramu ni nini?

Mamogramu ya uchunguzi ni Eksirei (picha dijito) ya tishu ya ndani ya titi la mwanamke. Mamogramu ya uchunguzi ndio mbinu bora zaidi ya kuchunguza saratani ya matiti mapema na huenda ikagundua saratani hiyo katika titi kabla ya wewe au daktari wako hata kuihisi.

Je, momogramu ya uchunguzi hufanywa vipi?

Titi linawekwa kwa umakini katika mtambo wa Eksirei na lina “bonyezwa” kwa sekunde chache huku Eksirei ikiwa inachukuliwa. Eksirei mbili zinachukuliwa katika kila titi, moja kutoka kwenye sehemu ya juu na nyingine kutoka kwenye sehemu ya upande. Kufinyizwa au “kubonyeza” kwa titi ni muhimu ili picha safi zaidi iweze kuchukuliwa na kiwango kidogo zaidi cha mnururisho kiweze kutumiwa. Kufinyiza kunaweza kuhisi kuwa kwenye kubana na kusikostarehesha, lakini kunadumu tu kwa sekunde chache kwa kila picha.

Nini hufanyika ninapotembelea BreastScreen SA?

Pindi unapoweka miadi yako, BreastScreen SA itakutumia “fomu ya Hojaji ya Kibinafsi na Kibali cha Uchunguzi” ambayo lazima uijaze na kuileta siku yako ya miadi.

Kwenye siku ya mamogramu yako, inapendekezwa uvae kuvalia vazi la vipande viwili kama vile sketi au suruali na shati na usitumie poda ya talcum au kiondoa harufu kwani hivi vinaweza kuathiri ubora wa picha ya Eksirei ambayo itapigwa.

BreastScreen SA inaelewa kwamba wanawake wengi huenda wakahisi wasiwasi kabla ya mamogramu yao, hata hivyo wafanyikazi wote wa kliniki ya BreastScreen SA ni wa kike na wanajali na kuheshimu mahitaji ya wanawake.

Wakati unawasili katika miadi yako kwenye kliniki ya BreastScreen SA

Tutakukaribisha, fomu yako ya kibali itaangaliwa na tuakujibu maswali yoyote ambayo huenda unayo. Tafadhali wasili dakika 10 mapema ili uweze kufidia muda huu. Utaonyeshwa chumba cha kubadilisha na kuombwa kuondoa vazi lako la sehemu ya juu. Unaweza kuomba gauni la kuvaa kwa muda na hatimaye kutupwa.

Mwanaradiografia wa kike atakupeleka kwenye chumba cha Eksirei ili kufanya mamogramu yako na pia kukuuliza maswali kadhaa. Eksirei za kila titi zitachukuliwa na kisha utakuwa huru kuondoka. Baada ya miadi yako ya uchunguzi Eksirei zako zitahakikiwa na madaktari wawili wataalamu (wanarediolojia) na utapokea matokeo ya kipimo chako kupitia kwa barua katika muda wa siku 14. Wakati mwingine mwanamke anaweza kuitwa ili kufanyiwa vipimo zaidi vikiwemo Eksirei, kipimo cha matiti na uchunguzi wa matiti kama kutakuwa na matokeo yoyote yasiyo ya kawaida katika mamogramu yako. Hii haimaanishi kwa kawaida kwamba unayo saratani ya matiti. Kama hii itahitajika basi mshauri mwuguzi kwenye BreastScreen SA atakupigia simu ili kujadili suala hili na wewe.

Itakuwaje kama ninayo historia ya familia ya saratani ya matiti?

Wanawake wa umri kuanzia 40 walio na historia thabiti ya familia kuhusu saratani ya matiti wanastahili kupata uchunguzi wa matiti wa bila malipo kila mwaka. Tupigie simu katika 13 20 50 ili kujadili hali zako za kibinafsi ili kuthibitisha kwamba unastahili kupata huduma hiyo.